

TAARIFA YA TATHMINI UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA PEMEBEJEO ZA KILIMO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE MWAKA 2015/2016

1.0. Utangulizi:

Kwa msimu wa mwaka 2015/2016 Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ilipokea jumla ya vocha **22,254** za ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa ajili ya kaya **7,418** za wakulima. Vocha hizo ambazo ni za mbolea ya kupandia, kukuzia pamoja na mbegu bora za mahindi chotara zilipokelewa kutoka ofisi ya Mkoa tarehe 9 Novemba, 2015 na kusambazwa katika vijiji vyote vya Halmashauri ndani ya muda wa siku tano (5) kama ilivyoelekezwa katika Waraka wa Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika kuhusu mkakati wa utekelezaji na usimamizi wa utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa wakulima kwa kutumia vocha wa mwaka 2015/2016. Orodha ya mchanganuo wa namba za vocha na idadi kwa kila kijiji umeambatanishwa pamoja na taarifa hii (**Kiambatisho Na.1**). Idadi, aina na thamani ya vocha za pembejeo zilizopokelewa na kusambazwa vijijini kwa msimu wa 2015/2016 ni kama zilivyoainishwa katika jedwali hapa chini.

***Jedwali Na.1:** Aina na idadi ya Vocha za pembejeo zilizopokelewa na kusambazwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwa msimu wa 2015/2016.*

NA.	AINA YA PEMBEJEO	VOCHA POKELEWA WILAYANI	VOCHA SAMBAZWA VIJIJINI.	THAMANI YA KILA VOCHA (TSH.)	JUMLA YA THAMANI YA VOCHA (TSH.)
1	<i>Mbolea ya Kupandia.</i>	7,418	7,418	35,000	259,630,000
2	<i>Mbolea ya Kukuzia.</i>	7,418	7,418	25,000	185,450,000
3	<i>Mbegu ya Mahindi Chotara.</i>	7,418	7,418	20,000	148,360,000
JUMLA		22,254	22,254		593,440,000

2.0. USAMBAZAJI WA PEMBEJEO ZA RUZUKU YA KILIMO VIJIJINI

Kamati ya Vocha ya Wilaya katika kikao chake cha tarehe 3 Septemba, 2015 ilijadili na kupitisha mapendekezo ya mgawanyo wa vocha katika vijiji vyote vya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, ikiwa ni pamoja na kujadili na kupitisha orodha ya jumla ya makampuni kumi na sita (16) yaliyoomba kusambaza pembejeo za ruzuku katika

Halmashauri. Makampuni yote yaliyopitishwa yalika bidhiwa mikataba ya usambazaji na Halmashauri kwa sharti la kuijaza na kuijeshwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri baada ya kukubaliana na masharti yaliyomo katika mikataba hiyo. Aidha makampuni yote yalipangiwa vituo vya kazi ndani ya Halmashauri na kutakiwa kuanza zoezi la usambazaji kwa haraka ili kuwahi msimu wa kupanda mazao kwa maeneo ambayo yalikuwa bado hayajachelewa msimu wa kupanda.

Hata hivyo kuna baadhi ya makampuni yaliyopangiwa kusambaza pembejeo kwa baadhi ya maeneo ambayo yameshindwa kurejesha mikataba ya Halmashauri na kuchelewesha usambazaji wa pembejeo katika maeneo hayo. Makampuni hayo ni:-

1. Minjingu Mines & Fertilizers Company Limited,
2. China Pesticides (T) Limited,
3. Meru Agro-Tours & Consultants Company Limited,
4. Bajuta International (T) Limited; na
5. MEA Fertilizers (T) Limited.

Makampuni kumi na moja (11) ya pembejeo yaliyosaini mikataba na Halmashauri na kuendelea na zoezi la usambazaji wa pembejeo hadi mwishoni mwa msimu wa kilimo ni kama ifutavyo:-

1. YARA Tanzania Limited,
2. Highland Seed Growers,
3. Tropical Seed (EA) Limited,
4. Tanzania Fertilizers Company Limited,
5. Premium Agrochemicals Limited,
6. Northern Seed Company Limited,
7. Kipato Seed Company Limited,
8. Rubuye Agrobusiness Company Limited,
9. Export Trading Company Limited,
10. Mohamed Enterprises (T) limited; na
11. Kibo Seed Trading & Services Limited.

Aidha kutokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwasili kwa vocha za pembejeo za ruzuku ya kilimo baada ya mazao kupandwa mashambani pamoja na wakulima wengi kwa baadhi ya vijiji kuwa na kipato duni hivyo kutokuwa na uwezo wa kuchangia sehemu ya pembejeo; jumla ya vocha **2,321** za pembejeo zilihamishiwa katika vijiji vyenye wakulima wenye uwezo wa kuchangia na kuchukua pembejeo hizo kabla ya msimu kuisha.

Hivyo hadi mwisho wa msimu wa kilimo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe jumla ya vocha zote **22,254** za ruzuku ya pembejeo za kilimo zenye thamani katika jedwali hapo juu kwa ajili ya kaya **7,418** za wakulima zimetumika.

3.0. MAFANIKIO KATIKA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA RUZUKU YA PEMBEJEO ZA KILIMO MWAKA 2015/2016

Miongoni mwa mafaniko katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo kwa mwaka 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

- i) Wakulima wengi katika vijijini wameelimika kuhusu umuhimu wa kutumia pembejeo, kwani kumekuwa na ongezeko la mahitaji kwa baadhi ya vijiji ambavyo wakulima walikuwa na uwezo wa kuchangia.
- ii) Pembejeo ziliweza kuwafikia wakulima katika vijiji vyao, hivyo kuwapunguzia wakulima gharama za usafiri na adhaa ya kuzifuata mbali na maeneo yao.
- iii) Wakulima walipata pembejeo kwa bei nafuu ikilinganishwa na bei halisi ya soko madukani.
- iv) Wakulima wamepata fursa ya kuunganishwa na makampuni mengi ya pembejeo na kufahamu ubora wa pembejeo zinazouzwa na makampuni mbalimbali nchini. Hivyo itawawezesha wakulima kuchagua pembejeo bora hata wakiwa nje ya mfumo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo.

4.0. CHANGAMOTO KATIKA ZOEZI LA USAMBAZAJI WA PEMBEJEO MSIMU WA 2015/2016.

Miongoni mwa changamoto zilizolikabili zoezi zima la usambazaji wa pembejeo vijijini kwa msimu wa 2015/2016 ni pamoja na hizi zifuatazo:-

- i. Kuchelewa kuwasili kwa vocha za pembejeo kutoka Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika hivyo kuathiri zoezi la usambazaji wa pembejeo kwa wakati kwa wakulima kulingana na jiografia ya Wilaya ya Rungwe. Hili limesababisha baadhi ya wananchi kugoma kabisa kuteuwa majina ya wanufaika wa pembejeo hizo. **Mfano:** Wananchi wa kitongoji cha Kisindile katika kijiji cha Isajilo kilichopo kata ya Mpuguso walioandika muhtasari wa kutokukubali kupokea vocha za pembejeo na kuuwasilisha kwa Serikali ya kijiji cha Mpuguso wakisistiza kuwa msimu wa kilimo kwao umeshapita, hivyo kutoona umuhimu wa kuzichukua pembejeo hizo.
- ii. Baadhi ya makampuni ya pembejeo yaliyoomba na kupitishwa kusambaza pembejeo kutosaini mkataba na Halmashauri na kuchelewesha usambazaji katika maeneo waliyopangiwa.
- iii. Kampuni ya pembejeo ya Mohamed Enterprises (T) Limited kupeleka mbolea zisizo na ubora katika kata ya Bujela.
- iv. Halmashauri kukosa mafuta ya usafiri wa kuwawezesha maafisa kilimo kusimamia zoezi la usambazaji na ugawaji wa pembejeo vijijini kwa karibu zaidi.
- v. Baadhi ya makampuni ya pembejeo kupanga bei kubwa zaidi ya bei ya soko ya pembejeo katika maeneo husika.
- vi. Baadhi ya wakulima walioteuliwa kuwa na uwezo mdogo wa kuchangia sehemu ya gharama ya pembejeo za ruzuku ya kilimo.